# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## KIKAO CHA KUMI NA TATU

**25 APRILI, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### KIKAO CHA KUMI NA TATU – TAREHE 25 APRILI, 2023

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MADINI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

## III. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**160. MHESHIMIWA SELEMAN JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Kituo cha Afya Bukene kitapatiwa mashine ya *X-Ray* na *Ultrasound*.

**161. MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON MAGESSA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Wananchi wa Busanda watapatiwa Wilaya ya Busanda kama ilivyopendekezwa na Baraza la Madiwani, DCC na RCC Geita.

## WIZARA YA AFYA:

**162. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itajenga Nyumba za Madaktari wa Hospitali ya Mkoa wa Iringa.

## WIZARA YA KILIMO:

**163. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mkakati gani wa kuwa na Sera ya kuongeza Tija katika Sekta ya Kilimo kwenye Mikoa ya Kanda ya Kati.

**164. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji wa Kyakakera uliopo katika Kata ya Kyaka.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**165. MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU (KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha Misamaha ya VAT inayotolewa inaleta tija kama ilivyokusudiwa.

**WIZARA YA MAJI:**

**166. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa mradi wa maji wa Kyerwa, Nyaruzumbura, Nyakatuntu hadi Kamuli Wilayani Kyerwa.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**167. MHESHIMIWA GODWIN EMMANUEL KUNAMBI (MLIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini vituo vidogo vya Treni vya Njage na Itongowa katika Reli ya TAZARA vitarejeshwa.

**168. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni hatua gani ya upembuzi yakinifu wa barabara ya Chimala, Matamba hadi Kitulo imefikiwa na lini ujenzi utaanza.

**169. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa Kivuko cha waenda kwa miguu katika eneo la Kisimani barabara kuu itokayo *Custom* kwenda Sumbawanga utaanza.

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

**170. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalinda Watoto walio tayari kwenye ndoa wakiwa na umri mdogo.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**171. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, lini Serikali itatangaza kumbukizi za Vita vya Majimaji vilivyoanzia Kijiji cha Nandete katika Gazeti la Serikali.

**WIZARA YA NISHATI:**

**172. MHESHIMIWA TAUHIDA CASSIAN GALLOS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, kuna mpango gani wa kukusanya madeni ya TANESCO katika Taasisi kubwa ili Shirika hilo liweze kujiendesha.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**173. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kuhusu Ndoa za Utotoni.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**174. MHESHIMIWA MAULID SALEH ALI (WELEZO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, kuna mkakati gani wa kudhibiti utapeli unaofanywa kwa kutumia namba za simu za nje.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc*** |
| **25 APRILI, 2023** | **KATIBU WA BUNGE** |